**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA RAIS**

**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

**HALMASHAURI YA WILAYA YA HANDENI**

# MUHTASARI WA KIKAO CHA KAWAIDA CHA KAMATI YA KUDUMU YA FEDHA, UONGOZI NA MIPANGO CHA TAREHE 30/11/2021

## WAJUMBE WALIOHUDHURIA

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 1. Mhe: Mussa I. Mwanyumbu | - | M/kiti wa Halmashauri | - | Mwenyekiti |
| 2. Mhe. Jasmin J. Paul | - | Makamu M/Kiti wa Halmashauri | - | Mjumbe |
| 3. Mhe: Nurdin S. Semnangwa | - | M/Kiti Kamati ya Huduma za Jamii | - | Mjumbe |
| 4. Mhe. Abdallah R. Pendeza | - | M/Kiti Kamati ya Huduma za Uchumi | - | Mjumbe |
| 5. Mhe. Onesmo A. Makomelo | - | Diwani Kata ya Segera | - | Mjumbe |
| 6. Bw. Saitoti Z. Stephen | - | Mkurugenzi Mtendaj (H/W) | - | Katibu |

## WAJUMBE AMBAO HAWAKUHUDHURIA

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 1. Mhe. John M. Sallu | - | Mbunge wa Jimbo | - | Kwa taarifa |
| 2. Mhe. Mwanaisha H. Mseni | - | Diwani Kata ya Sindeni | - | Kwa taarifa |

## 3. WATAALAMU WALIOHUDHURIA.

| | | |
|---|---|---|
| 1. Bw. Charles A. Mwaitege | - | Mkuu wa Idara ya Utumishi na Utawala |
| 2. Bw. Yibarila C. Kamele | - | Mkuu wa Idara ya Kilimo, Umwagiliaji na Ushirika |
| 3. Bw. Aidan Angetile | - | Mkuu wa Idara ya Fedha na Biashara |
| 4. Bi. Rachel L. Mbelwa | - | Mkuu wa Idara ya Maendeleo ya Jamii |
| 5. Bw. Erasto Mligo | - | Kaimu Mkuu wa Idara ya Ardhi na Mipangomiji |
| 6. Bw. Saturine J. Kessy | - | Mkuu wa Kitengo cha Ukaguzi wa ndani |
| 7. Wakili Amani H. Mangesho | - | Mkuu wa Kitengo cha Sheria |
| 8. Mwl. Goodluck Mwampashe | - | Mkuu wa Idara ya Elimu Msingi |
| 9. Bw. Napoleon Mlowe | - | Mkuu wa Idara ya Maliasili |
| 10. Bw. Brian J. Munga | - | Kaimu Mkuu wa Kitengo cha Manunuzi |
| 11. Bw. Richard J. Ngambeki | - | Kny. Mkuu wa Idara ya Ujenzi |
| 12. Bw. Sekiara Kiariro | - | Mkuu wa Idara ya Mifugo na Uvuvi |
| 13. Bi. Amina K. Saidi | - | Mkuu wa Idara ya Mipango, Takwimu na Ufuatiliaji |
| 14. Dr. William Awe | - | Kny. Mkuu wa Idara ya Afya |
| 15. Bw. Leonard D. Mkayullah | - | Kaimu Mkuu wa Idara ya Mazingira na Udhibiti wa Taka ngumu |
| 16. Bw. Venance J. Ntandu | - | Kaimu Mkuu wa Kitengo cha TEHAMA |
| 17. Bw. Elinihaki Hashimu | - | Kaimu Mkuu wa Kitengo cha Ufugaji Nyuki |
| 18. Mwl. Fadhili R. Mdee | - | Katibu Tume ya Utumishi wa Walimu (W) |
| 19. Bi. Amina H. Luhizo | - | Mratibu TASAF |
| 20. Bi. Amina Waziri | - | Mratibu UKIMWI (W) |
| 21. Bw. Francis E. Mashalo | - | Mkuu wa Kitengo cha Uchaguzi |
| 22. Bw. Nathanael George | - | Kny. Mkuu wa Sehemu ya Ushirika |

23. Bi. Salvina D. Swaga - Afisa Biashara
24. Bw. Salim Mkilindi - Mhasibu Mapato
25. Bw. Sprian Luanda - Afisa Habari wa Halmashauri
26. Bw. Hatibu Stambuli - Afisa Elimu Vifaa na Takwimu Sekondari

**SEKRETARIETI**

1. Bw. Selemani M. Mhunga - Mwandishi wa Mikutano

**MUHTASARI NA. 73/2021/2022:- KUFUNGUA KIKAO**

Katibu aliwaeleza wajumbe, hicho ni kikao cha kawaida cha Kamati kwa ajili ya kupokea na kujadili taarifa za Mapato na Matumizi ya Fedha za Halmashauri katika kipindi cha mwezi Oktoba, 2021. Baada ya maelezo alimwomba Mwenyekiti afungue kikao na Mwenyekiti alifungua kikao saa 04:58 asubuhi.

**MUHTASARI NA. 74/2021/2022:- KUTHIBITISHA AGENDA**

Katibu aliwasilisha agenda zilizoandaliwa ambazo ni:-

1. Kufungua kikao.
2. Kuthibitisha agenda.
3. Kusoma na kuthibitisha muhtasari wa kikao cha Kamati ya Fedha, Uongozi na Mipango kilichofanyika tarehe 01/11/2021.
4. Taarifa ya utekelezaji wa maagizo ya kikao cha Kamati ya Fedha, Uongozi na Mipango kilichofanyika tarehe 01/11/2021.
5. Taarifa ya Mapato na Matumizi ya fedha za Halmashauri katika kipindi cha mwezi Oktoba, 2021.
6. Taarifa ya wadaiwa (Defaulters) wa makusanyo ya mapato ya ndani ya Halmashauri Mwezi Oktoba 2021.
7. Taarifa ya mapokezi ya fedha kiasi cha shilingi 2,255,445,822.51 nje ya mpango na bajeti ya Halmashauri kwa mwaka 2021/2022.
8. Mengineyo kwa idhini ya Mwenyekiti.
9. Kufunga kikao.

Kamati ilipitia agenda zilizowasilishwa na kuridhia zijadiliwe.

**MUHTASARI NA. 75/2021/2022:- KUSOMA NA KUTHIBITISHA MUHTASARI WA KIKAO CHA KAMATI YA FEDHA, UONGOZI NA MIPANGO CHA TAREHE 01/11/2021**

Muhtasari wa kikao cha Kamati ya Fedha, Uongozi na Mipango cha tarehe 01/11/2021 ulisomwa na wajumbe kuupokea na kuuthibitisha ili uwe kumbukumbu ya vikao vya Kamati.

**MUHTASARI NA. 76/2021/2022:- TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA MAAGIZO YA KIKAO CHA KAMATI YA FEDHA, UONGOZI NA MIPANGO CHA TAREHE 01/11/2021.**

Kamati ilifahamishwa kwamba hakuna maagizo yoyote yaliyobainika kutokana na muhtasari wa kikao cha Kamati ya Fedha, Uongozi na Mipango kilichofanyika tarehe 01/11/2021.

**MUHTASARI NA. 77/2021/2022:- TAARIFA YA MAPATO NA MATUMIZI YA FEDHA ZA HALMASHAURI KATIKA KIPINDI CHA MWEZI OKTOBA, 2021**

Mkuu wa Idara ya Fedha na Biashara kwa niaba ya Mkurugenzi Mtendaji Wilaya aliwasilisha taarifa ya Mapato na Matumizi ya fedha za Halmashauri katika kipindi cha mwezi Oktoba, 2021 na wajumbe kuipokea.

**a) Mapato halisi mwezi Oktoba, 2021**

| Maelezo ya kasma | Makisio 2021/2022 | Mapato halisi mwezi Julai hadi Septemba, 2021 | Mapato halisi mwezi Oktoba, 2021 | Jumla ya Mapato halisi mwezi Julai hadi Oktoba, 2021 | % |
|---|---|---|---|---|---|
| Mapato ya Ndani (Own Source) | 2,175,903,566.00 | 512,297,797.30 | 208,423,728.02 | 720,721,525.32 | 33 |
| Mishahara | 34,311,213,097.00 | 5,246,309,514.00 | 1,736,937,800.00 | 6,983,247,314.00 | 20 |
| Matumizi Mengine - OC | 1,005,709,000.00 | 294,322,249.95 | 29,800,748.00 | 324,122,997.95 | 32 |
| Miradi ya Maendeleo | 18,097,480,874.00 | 2,873,459,435.41 | 2,485,352,480.00 | 5,358,811,915.41 | 30 |
| Jumla ya Mapato | **52,798,544,971.00** | **8,926,388,996.66** | **4,460,514,756.02** | **13,386,903,752.68** | **25** |

**b) Matumizi halisi mwezi Oktoba, 2021**

| Maelezo ya kasma | Makisio 2021/2022 | Matumizi halisi mwezi Julai hadi Septemba, 2021 | Matumizi halisi mwezi Oktoba, 2021 | Jumla ya Matumizi halisi mwezi Julai hadi Oktoba, 2021 | % |
|---|---|---|---|---|---|
| Mapato ya ndani ( Own Sorce) | 2,175,903,566.00 | 186,248,178.67 | 64,602,928.00 | 250,851,106.67 | 12 |
| Mishahara | 34,311,213,097.00 | 5,246,309,514.00 | 1,736,937,800.00 | 6,983,247,314.00 | 20 |
| Matumizi mengine OC | 1,005,709,000.00 | 82,431,638 | 398,647,167.00 | 481,078,805.00 | 48 |
| Miradi ya maendeleo | 16,027,480,874.00 | 26,500,000.00 | 353,323,048.00 | 379,823,048.00 | 2 |
| **Jumla matumizi** | **52,798,544,971.00** | **5,541,489,330.67** | **2,553,510,943.00** | **8,095,000,273.67** | **15** |

Kamati ilijadili taarifa ya Mapato na Matumizi ya fedha za Halmashauri katika kipindi cha mwezi Oktoba 2021, kwa kutaka kupatiwa ufafanuzi wa namna Halmashauri inavyokusanya ushuru wa zao la Mkonge hasa kwa wakulima binafsi wanaolima zao hilo, kwani uchakataji wa zao hilo hufanyika Wilaya ya Korogwe.

Mkuu wa Idara ya Fedha na Biashara kwa niaba ya Mkurugenzi Mtendaji Wilaya akitoa ufafanuzi alikifahamisha kikao kuwa ushuru huo zinatozwa kwa mujibu wa sheria ndogo ya Halmashauri ya ushuru wa zao la mkonge. Ushuru huo unatozwa kwa namna mbili:-

i. Zinatozwa kwa meta moja ya ujazo kwa majani mabichi ya mkonge ambapo meta moja ya ujazo inatozwa kwa shilingi 1,080.00

ii. Zinatozwa kwa tani moja ya nyuzi za mkonge baada ya kuchakatwa ambapo tani moja inatozwa kwa shilingi 37,802.86

Kwa kuwa Bodi ya Mkonge imeweka taratibu za kudhibiti mapato ya Serikali kwa kuwataka wasafirishaji kulipa ushuru kwenye maeneo yaliyozalisha mkonge huo, hivyo takwimu za mauzo hupatikana viwandani na ulipwaji wa ushuru hufanyika huko.

Pamoja na majibu ya Menejimenti, Kamati ilionesha wasiwasi kuhusiana na uhalisia wa takwimu zitolewazo viwandani. Kutokana na wasiwasi huo, na kwa kuwa Sheria ya Barabara inaruhusu Wahifadhi Misitu Tanzania (TFS) kuweka vizuizi vya ukaguzi wa mazao ya misitu kwenye maeneo ya barabara kuu, Kamati ilishauri Menejimenti itumie mbinu zilizotumiwa na Watendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Korogwe ifanye mawasiliano na TANROADS Mkoa na TFS kuazisha vizuizi vya kukusanyia mapato katika eneo la Mailikumi na Vigae (mpakani mwa Handeni na Korogwe) ili vitumike kufuatilia na kupata takwimu halisi za magari yanayosafirisha majani ya mkonge kwenda viwandani.

Katika kuongeza mapato katika Kata ya Kitumbi ambayo mapato yake yapo chini zaidi ilishauriwa yafuatayo yafanyiwe kazi:-

i. Menejimenti ifuatilie na kuweka POS kwenye barabara inayotumika kusafirisha madini ya ujenzi kutoka kwenye mgodi kabla ya kuingia barabara kuu ili kudhibiti mapato ya chanzo hicho.
ii. Eneo la Kitongoji cha Lugala Kata ya Kitumbi kunazalishwa mkaa, mbao na magogo mengi hivyo Menejimenti iweke juhudi za makusudi za kufuatilia eneo hilo.
iii. Kamati ya Mapato ikishirikiana na walezi wa Kata ifanye juhudi za makusudi za kufuatilia mapato katika Kata za Sindeni na Kwamatuku ambazo hadi mwezi Oktoba, 2021 zimekusanya kwa asilimia 8.

Baada ya majadiliano, Kamati iliipitisha taarifa ya Mapato na Matumizi ya fedha za Halmashauri katika kipindi cha mwezi Oktoba, 2021.

**MUHTASARI NA. 78/2021/2022:- TAARIFA YA WADAIWA WA MAKUSANYO (DEFAULTERS) WA MWEZI OKTOBA, 2021**

Mkuu wa Idara ya Fedha na Biashara kwa niaba ya Mkurugenzi Mtendaji Wilaya aliwaeleza wajumbe kuwa katika kipindi cha Mwezi Oktoba, 2021 wakusanyaji wote walisimamiwa vizuri na kuweza kuwasilisha fedha za makusanyo yote benki, hivyo hakuna wadaiwa wa mapato katika kipindi hicho.

Kamati iliipongeza Menejimenti kwa ufuatiliaji na ushirikiano mzuri uliopo kati yao na Maafisa Watendaji wa Kata pamoja na wakusanyaji vituoni. Ilishauriwa ushirikiano huo uendelee katika miezi inayofuata ili kuondoa kabisa changamoto ya wadaiwa wa mapato katika mifumo ya mapato ya Halmashauri.

**MUHTASARI NA. 79/2021/2022:- TAARIFA YA MAPOKEZI YA FEDHA KIASI CHA SHILINGI 2,255,445,822.51 NJE YA MPANGO WA BAJETI YA HALMASHAURI KWA MWAKA WA FEDHA 2021/2022.**

Mkuu wa Idara ya Mipango, Takwimu na Ufuatiliaji kwa niaba ya Mkurugenzi Mtendaji Wilaya aliwasilisha taarifa ya mapokezi ya fedha kutoka Serikalini kiasi cha shilingi 2,255,445,822.51

nje ya mpango wa bajeti ya Halmashauri kwa mwaka wa fedha 2021/2022 na wajumbe kuipokea.

Akiwasilisha aliwaeleza wajumbe kuwa Halmashauri ya Wilaya ya Handeni mnamo tarehe 16/11/2021 iliingiziwa fedha kiasi cha shilingi 2,255,445,822.51 nje ya bajeti ya mwaka wa fedha 2021/2022 (Fedha za UVIKO 19 Tshs. 435,445,822.51 ziliingizwa kwenye akaunti ya Halmashauri nje ya bajeti ya mwaka wa fedha 2021/2022, Tshs. 1,440,000,000.00 ziliingizwa moja kwa moja kwenye akaunti za shule kwa ajili ya ujenzai wa madarasa ya shule za sekondari na Tshs. 380,000,000.00 kwa ajili ya ujenzi wa madarasa ya shule shikizi). Mchanganuo wa fedha hizo ni kama ifuatavyo:-

| | | | |
|---|---|---|---|
| i. | Kiasi cha shilingi 38,931,075.51 | - | Ufuatiliaji wa chanjo ya UVIKO 19. |
| ii. | Kiasi cha shilingi 300,000,000 | - | Majengo ya huduma za dharura Hospitali ya Wilaya. |
| iii. | Kiasi cha shilingi 90,000,000 | - | Nyumba za watumishi wa Afya katika Hospitali ya Wilaya. |
| iv. | Kiasi cha shilingi 6,514,747 | - | Ufuatiliaji na tathimini ya miradi ya UVIKO 19 (Madarasa shule za sekondari na shikizi, miradi ya majengo ya huduma za dharura na nyumba za watumishi wa Afya). |
| v. | Kiasi cha shilingi 1,440,000,000 | - | Ujenzi wa madarasa ya kupokea wanafunzi wa kidato cha kwanza 2022. |
| vi. | Kiasi cha shilingi 380,000,000 | - | Ujenzi wa madarasa ya shule shikizi |

Kwa kuwa fedha za UVIKO 19 na ujenzi wa madarasa zililetwa nje ya bajeti na kwa kuwa kwenye mpango na bajeti ya Halmashauri ya mwaka 2021/2022 hakuna vifungu vya matumizi ya fedha hizo, aliwasilisha maombi ya idhini ya kupatiwa vifungu ili kuweza kufanya matumizi.

Kamati ilipokea, ilijadili na kuipitisha taarifa ya mapokezi ya fedha kutoka Serikalini kiasi cha shilingi 2,255,445,822.51 nje ya mpango na bajeti kwa kushauri kuwa Menejimenti ifuate taratibu ili kupatiwa vifungu vya matumizi. Hata hivyo ilipongeza Serikali kwa hatua hiyo ya kuleta fedha za utekelezaji wa miradi ya maendeleo kwani inaisaidia jamii katika kujiletea maendeleo ya haraka.

**MUHTASARI NA. 80/2021/2022:- MENGINEYO KWA IDHINI YA MWENYEKITI.**

**i. Vitambulisho vya Waheshimiwa Madiwani**

Waheshimiwa Madiwani walitaka kufahamishwa kuwa Menejimenti itafamikisha lini suala la vitambulisho vyao, kwani changamoto hiyo limekuwa ikiwasumbua wakati wa utekelezaji wa majukumu yao maeneo yaliyopo nje ya Halmashauri.

Mkuu wa Idara ya Utumishi na Utawala kwa niaba ya Mkurugenzi Mtendaji Wilaya alitoa ufafanuzi wa hoja kwamba Menejimenti imeshaanza kulifanyia kazi katika hatua za awali za kumtafuta Mzabuni wa kazi hiyo.

Kamati ilishauri mchakato wa upatikanaji wa vitambulisho uharakishwe ili kuondoa changamoto hiyo kwa Waheshimiwa Madiwani.

**ii. Halmashauri kufuata taratibu za Uteuzi wa nafasi za kukaimu Ukuu wa Idara na Vitengo**

Kamati ilifahamishwa kuhusiana na maelekezo ya Naibu Waziri, Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora kupitia ziara yake iliyofanyika Wilayani Handeni tarehe 29/11/2021 kuhusiana na Halmashauri kufanya uteuzi wa Wataalamu wenye sifa za kukaimu nafasi za Wakuu wa Idara na Vitengo kwa lengo la kujaza nafasi wazi kwa kufuata Sheria, Kanuni na Taratibu zilizopo.

Katika maelekezo hayo alizitaka Mamlaka za Nidhamu na Uteuzi za Watumishi kuhakikisha zinaomba vibali na kupatiwa Barua za Uteuzi huo kutoka kwa Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora badala ya barua za Wakurugenzi Watendaji wa Halmashauri.

Mkuu wa Idara ya Utumishi na Utawala kwa niaba ya Mkurugenzi Mtendaji Wilaya akitoa ufafanuzi alikifahamisha kikao kuwa suala hilo hujadiliwa kwa SIRI, hivyo alishauri lijadiliwe kwenye kikao cha Kamati kitakachofanyika mwezi Disemba, 2021 baada ya kupata ridhaa kutoka kwa Katibu wa Baraza la Madiwani (Mkurugenzi Mtendaji Wilaya).

**MUHTASARI NA. 80/2021/2022:- KUFUNGA KIKAO.**

Mwenyekiti aliwashukuru wajumbe na wataalamu kwa kujadili agenda zilizowasilishwa. Baada ya maelezo Mwenyekiti alifunga kikao saa 08.52 Mchana.

**MUHTASARI UMETHIBITISHWA**

| **KATIBU** | **MWENYEKITI** |
|---|---|
| **JINA:** Bw. Saitoti Z. Stephen | **JINA:** Mhe: Mussa I. Mwanyumbu |
| **SAINI:** P.P ........................ | **SAINI:** ........................ |

**TAREHE:** 07/12/2021